



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY – FOURTH SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 14th October 2020

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 3.30 p.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

PAPERS

THE COUNTY BUDGET REVIEW AND OUTLOOK PAPER 2020

The Leader of Majority (Hon. Mwathethe): Thank you Mr. Speaker. I wish to lay on the Table of this House, the County Budget Review and Outlook Paper 2020. Thank you, Mr. Speaker.

(Hon. Mwathethe laid the Paper on the Table)

NOTICE OF MOTION

ESTABLISHMENT OF THE COUNTY ATTORNEY OFFICE

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you, Mr. Speaker for this consideration; I appreciate. I rise to give a Notice of Motion to the County Executive Committee Member in-charge of Devolution, Public Service and Disaster Management:-

THAT, AWARE THAT , the Office of the County Attorney Act 2020, establishes the Office of the County Attorney, County Solicitor and County Legal Counsels.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

FURTHER AWARE THAT, the Act provides for the appointment of the County Attorney by the Governor with the approval of the County Assembly but the rest of the officers are to undergo a competitive recruitment process through the County Public Service Board.

NOTING WITH CONCERN THAT, Section 31 of the Act provides for transition of office and officers that existed prior to the Act coming to effect.

This honourable House therefore urges the County Secretary to operationalize the County Attorney Act 2020, through the appointment of the County Attorney by the Governor and forwarding the name to the County Assembly for vetting and secondly, undertake a competitive recruitment process for the positions of the County Solicitor and County Legal Counsels as per the Act.

MOTION

DISTRIBUTION OF SANITARY TOWELS TO ADOLESCENT GIRLS IN THE COUNTY

Hon. (Ms.) Koki: Thank you Mr. Speaker. I beg to move a Motion to the County Executive Committee Members in-charge of Health Services and Gender, Culture, Social Services and Sports Departments:-

THAT, AWARE THAT, Kilifi County records extremely high cases of pregnancies among teenage girls with an estimated 18.4 percent of girls aged 15 to 19 years in Kenya reported to have began child-bearing. Out of this, 21.8 percent are from Kilifi County. (The Change Initiative (TCI) report 2019).

AWARE THAT, lack of sanitary towels among the teenagers has highly contributed to the engagement of this vice with reports indicating that girls from poor and underprivileged communities end up in transactional sexual relationships with men for sanitary towels and other basic needs. The Basic Education Amendment Act, 2017 mandates the National Government to provide free, sufficient, quality, sanitary towels to every girl-child registered and enrolled in a public basic education institution and have reached puberty but this initiative has been marred with inconsistency in distribution forcing local organizations and well-wishers to step in and salvage the situation.

NOTING WITH CONCERN THAT, the COVID-19 pandemic has worsened the situation, putting more teenage girls at risk of engaging in immoral sexual relations which in turn raises the number of early pregnancies within the County.

This honourable House therefore urges the County Government's Departments in-charge of Health Services and that of Gender, Culture, Social Services and Sports to come up with community programmes aimed at distributing sanitary towels and educating the adolescent girls on menstrual hygiene.

Before I call my Seconder, I would want to give my submission on the same. Sanitization and hygiene occupy the most important space in the Kenyan Constitution. I would want to give my submission as follows; I will give an analysis. Menstrual hygiene and lack of sanitary towels remains a thorn in the flesh particularly to school going children. In a number of counties, initiatives have been spread out through the Departments of Gender and that of Health Services to come with programmes and projects aimed at restoring dignity of girls through menstrual awareness and distribution of such initiatives. I will give a few examples of such counties; Mombasa County runs a programme of sanitary distribution to school-going girls. In 2020, a Motion was sponsored by hon. Milka in the County Government of Mombasa. In Murang'a

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

County, a Motion was raised by MCA (Member of County Assembly) Mary Waithaya. Tana River introduced Health Clubs both in primary and secondary schools.

The reason why I brought this Motion is if you all know what I do in the community, I hold the girl child close to my heart. I did not start the initiative of distributing towels during this pandemic but I started this initiative way back in 2013. We have gone round within Kilifi County and around 8,000 girls have benefitted from this initiative but it's sad to say that we feel we are not really doing enough because we are still not getting to all the girls who require the sanitary towels. I will give an example; during this pandemic, we have already moved to about three wards within Kilifi County and it is sad to say in this era you go to a ward and you give dignity packs to a girl and this girl talks to you with a lot of sadness that this is the time that she is seeing a sanitary towel for the first time in her life. This is a story of a girl who is in form three saying that she is seeing a sanitary towel for the first time.

During our initiatives when we go out to the communities, we talk to these girls and we ask them really if your parents cannot afford sanitary towels then where do you get the sanitary towels from? Some of them were open enough to say they trade sex for sanitary towels. It is sad. Our girls are trading sex for sanitary towels in this county.

Some of the girls also said that sometimes they get the sanitary towels in the schools and sometimes they do not. This Bill was assented to by the President that school going girls in public schools should be given sanitary towels. We don't see it happening.

It is sad that in this era a girl can miss school because of lack of sanitary towels. In one of the wards, we found that some girls were even telling us that they cut mattresses, they use *lessos* and some say they dig holes. This is something we saw on National TV (television) in our neighboring county. I want to tell this House that this thing is happening in Kilifi County and as hon. Members, let us leave here in 2022 saying we have not done everything for the people of Kilifi but we have given dignity to the girls of Kilifi County because we are going to lose a future generation. Leave alone the early pregnancies that we are experiencing especially now during this COVID-19, those girls are going to get a lot of infections. A girl who gets pregnant means they have slept with a man without protection. Let's forget about the early pregnancies and think about HIV (Human Immuno-deficiency Virus). Let us think about all those diseases. We are going to lose a generation and those are the MPs, MCAs, doctors that we are looking at having here in Kilifi County. A survey conducted by the Change Initiative in 2019 revealed that school going children succumbed to early unplanned pregnancies due to lack of sanitary towels.

Kilifi County sums up to 21.8 percent of girls countrywide between the ages of 15 and 19 years who have started child bearing. It is expected that the numbers must have risen greatly due to the COVID-19 pandemic which has left school-going children to stay at home and inadequate supply of sanitary towels in schools cut off completely during the period of the pandemic.

Several other studies carried out have pointed to lack of access to sanitary towels as a key contributor to early pregnancies, marriages and eventually drop out from schools.

The three Departments mentioned above have community programmes that respond to the prayer of the Motion. The Department of Health has reproductive health programmes while the Gender Department has budgeted for public campaigns. It will therefore be prudent for them to have assurance of sanitary towels and hygiene be incorporated in such programmes since the issue of magnitude of the COVID-19 pandemic and the ripple effects of the teenage girls call for prompt measures such as coming up with innovative programmes aimed at distributing sanitary towels and educating the adolescent child about hygiene.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, as I have said in my statement before, a girl child is close to my heart. I would want to ask this honourable House to support this Motion. If the President assented to the Bill that school-going girls should be given sanitary towels and we are not seeing it happen, if it is happening then it is not reaching all the corners of this county. These two Departments can set aside money and those girls can be given the sanitary towels. They can come up even with school clubs; whichever way so that we can have these girls not trading sex for sanitary towels. If one of the reasons why we are having so many cases of early pregnancies in Kilifi County is poverty and lack of sanitary towels, then if we solve this problem we will see if we will have any other reasons why our girls are getting pregnant at an early stage.

If we do not solve one problem after another, then we shall keep on talking about poverty and we shall keep on talking about lack of sanitary towels while we are not solving problems. If we solve this one by issuing school-going girls with sanitary towels, we will know the reason why our girls are getting pregnant at an early age or are there another reasons?

So, I am humbly asking this honourable House to support me in pushing this Motion. I would want to leave this House knowing no girl will miss going to school because of lack of sanitary towels. May I call upon hon. Mwayaa to support this Motion. Thank you.

(Hon. Mwayaa seconded)

(Question proposed)

Hon. Mwayaa: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Naunga mkono yale ambayo mheshimiwa Koki ameyaongea. Acha pia nikupongeze mheshimiwa Koki ukiwa wewe ni mheshimiwa wa kwanza mwananake hapa Kilifi ambaye tumekuona una mfano mzuri. Mheshimiwa Koki ameanzisha *foundation* yake mwenyewe ikiitwa Kadzo Foundation ambayo anaenda wadi baada ya nyengine akipeana hizo *sanitary towels* yeye kama mheshimiwa. Leo hii ameleta Hoja katika Bunge hili ili tumuunge mkono hili jambo likachukuliwa liwe la Kaunti ya Kilifi.

Kaunti ya Kilifi imerekodi mimba nyingi za mapema na ukiangalia miaka ya nyuma tumeenda vitongoji tofauti tofauti vya Kilifi pamoja na Gavana wetu tukipeleka habari ya kwamba Kilifi inaelekea pabaya kwa ajili ya mimba za mapema lakini Biblia inasema ya kwamba imani bila matendo imekufa. Mheshimiwa Koki sasa ameleta matendo kwamba injili ihubiriwe mimba za mapema hazifai zitatupeleka pabaya na vile vile tuwasaidie wasichana wetu kuwapatia zile sodo kwa wakati unaofaa ili wakae madarasani.

Katika wakati huu ambao tunaona kuna janga la Corona, wazazi wetu na watu wengi wamekosa kazi. Wengine wamesimamishwa kazi na wengine vibarua walivyokuwa wametumainia vimefilisika kwa ajili ya janga la Corona. Naomba mswada huu upitishwe ili kwamba wale wazazi ambao wako chini kwa sababu kazi zao ziliisha kwa ajili ya Corona wasaidike baada ya Mswada huu kupita. Tutatenga kiwango cha pesa cha kununulia sodo wasichana wetu wa shule.

Mheshimiwa Spika, wacha nishukuru Bunge hili na hata lile Bunge la kwanza maana tumepitisha Mswada ambao umesaidia sana mtu ambaye anaishi katika Gatuzi la Kilifi. Ukiniruhusu mheshimiwa Spika, nitataja mawili ama matatu; tumepitisha Mswada wa *Scholarship* ili insaidie mwanafunzi ambaye anakosa karo katika gatuzi la Kilifi. Tumefaulu kwa sababu ukiangalia tumesaidia wale ambao familia zao ziko chini na hawawezi kufundisha

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

watoto wao. Ndio maana hata saa hii tumeona Koki ameleta Mswada huu ili tuweze kupeleka kwa msichana ambaye haweza kufikia masomo yake kwa ajili ya hivi vitu.

Tukaleta Mbegu Fund na tukaipitisha; Mbegu Fund inasaidia mtu wa Gatuzi la Kilifi. Pongezi mheshimiwa Koki kwa kuleta Mswada katika Bunge hili ili tuwe na mfuko ambao utalenga mtoto wa kisichana asiingie katika anasa na tupate wasichana wengi ambao wamesoma. Kama Mheshimiwa Kenga alivyoleta ile *Statement* yake ya kusema madaktari wengi wako nje, pengine wale wangeingia mimba mapema hawangukuwa madaktari. Pongezi na naunga mkono mheshimiwa Spika. Asante sana.

Hon. (Ms.) Mwangome: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Nataka nimpongeze mheshimiwa Koki kwa kuleta huu Mswada. Naunga mkono hili jambo lipite na wasichana wetu wasaidike. Kwa ruhusa yako mheshimiwa Spika nitoe tu mfano kidogo; pale kwangu nimeletewa msichana yapata wiki moja saa hii nikiendelea kumhoji na kuongea naye. Alikuwa anaishi kule mpaka wa Tana River na Kilifi. Msichana alitoroka kule alikokuwa anaishi maana wazazi wake walifariki na akachukuliwa na *relatives* lakini yule *relative* anaishi kilomita kumi (10) kutoka anakoishi yule msichana huku ameachiwa watoto wadogo yeye kama mlezi na yeye mwenyewe ni msichana wa shule yuko kidato cha pili. Msichana alipoona hali inakuwa ngumu alitoroka na akafika kwa *relative* wake kule Chasimba na akawa analia kila siku hajulikani ni nini kinamliza. Aliletwa mpaka pale kwangu na nikawa najaribu kumhoji. Akanisimulia jambo la kusikitisha sana. Msichana huyu aliachwa na mwanamme ambaye hana bibi, yuko na watoto watano na msichana huyo ndiye anayeangalia watoto akienda shule asubuhi na jioni. Namuuliza ulikuwa ukipata wapi vitu vyako vya kutumia analia kusema ni hali ngumu nitakuelezea nikipata nguvu ya kuongea.

Naona ni jambo la muhimu sana tupitisha mswada huu waheshimiwa wenzangu kwa haraka ili tusaidie wasichana wetu. Pia ningemuomba mheshimiwa Koki afike wadi ya Chasimba; kuna wasichana wengi ambao wanahitaji msaada na pia nikuulize kama unaweza kuja kuongea nao kama mwenye kuanzisha hii *foundation* ili tusaidiane wasichana wasaidike. Asante sana mheshimiwa Spika.

Hon. Ziro: Asante sana mheshimiwa Spika. Nami nimesimama ili kuweza kumuunga mkono mheshimiwa aliyelea Mswada huu. Ni jambo la kusikitisha kwamba mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Kenya aliweza kutia sahihi katika hii *Act* ambayo inaruhusu serikali kuu kupatiana sodo bure na za kutosha na pia ambazo zimethibitika...

Hon. Kenga: Point of Information...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Peter Ziro, do you wish to be informed?

Hon. Ziro: Yes, information is power, Mr. Speaker.

Hon. Kenga: Mheshimiwa Spika, nieleze tu mheshimiwa Peter Ziro na waheshimiwa wengine wanaochangia kwamba mheshimiwa Koki hajaleta Mswada; ni Hoja ambayo iko mbele yetu tunajadili. Nimesikia wengi wakiongea kuhusu 'Mswada' ilhali ni 'Hoja' ambayo iko mbele yetu katika Bunge kwa ajili ya kuijadili.

Hon. Ziro: Asante kwa hayo marekebisho. Nilikuwa nasema kwamba ni jambo la kusikitisha kuona kwamba mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Kenya aliweka saina katika sheria hii, katika *guidelines* ambazo zinapeana uhuru wa serikali kuu kupeana sodo bure za kutosha na pia zilizohibitika kwa watoto wote ambao wako katika shule za msingi ambao ni wasichana ambao wamebalehe. Lakini kufikia sasa vifaa hivi muhimu labda vinafikia watu wachache sana haswa tukiangalia katika jimbo letu la Kilifi.

Nataka nimuunge mkono mheshimiwa Koki kwa sababu ya bidii zake ambazo amezifanya kuweza kuleta Hoja hii. Mimi mwenyewe ni shahidi. Wakati wa mafuriko alitembea

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kutoka sehemu anayokaa mpaka akafika katika wadi yangu ya Garashi na akaja akagawanyia wasichana wale ambao walikuwa wanatatizika kupata sodo hizi. Kwa hivyo, najua ndani ya moyo wake yuko na ule utu wa kuweza kusaidia msichana mwenzake kwa sababu yeye ni msichana ni lazima amepitia hali kama hizo. Na akiwa amepitia hali kama hizo nafikiri ndio mtu ambaye ni wa hakika na wa sahihi kuweza kutueleza na ameonyesha ule uchungu ambao amepitia kwa kuleta Hoja hii ndani ya Bunge hili ili tuweze kuiunga mkono na kuipitisha.

Hivi tunavyozungumza, kule kwangu niko na kesi moja ya msichana ambaye alilazimishwa na kijana kwa sababu alikuwa akimpatia zawadi kama hizi na akamlazimisha kulala na yeye mpaka mwisho yule msichana aka *overbleed* na akafariki. Hiyo kesi iko kortini na inaendelea na ni jambo la kusikitisha. Kama kungekuwa na mipangilio kabambe ya serikali yetu ya kaunti hasa kwa hii Idara yetu ya *Gender* na Afya zishikane pamoja ili kwamba vifaa muhimu kama hivi vipelekwe kwa wale wasichana ili wasaidike. Ninaamini hata kama haitamaliza kabisa haya mambo ya mimba za mapema na wasichana wetu kudhulumiwa kimapenzi na vijana lakini itapunguza, maana katika jamii yetu sisi wagiriana tuna msemu mmoja ambao unasema; na kama mheshimiwa Spika utaniruhusu nitausema hapa. Naomba kwa sababu sina maneno mwafaka ambayo naweza kuyatumia kwa Kiingereza ama Kiswahili kuelezea msemu huo.

(Loud consultations)

Hata nadhani ni Kiswahili maana wanasema *kaluhanga ni kaluhanga*, si ni Kiswahili hicho?

(Laughter)

Ni Kiswahili cha ndani. Yaani yule ambaye ni kuenda na mwewe ataenda tu hata ukamficha vipi. Ndio nilikuwa nataka kueleza kwamba hawa wasichana wetu hata kama tutawasaidia kuna wale ambao washaamua, lakini tunapoleta hizo sodo itapunguza kwa asilimia kubwa sana na hawa wasichana wetu waendeleo na masomo. Vile vile itapunguza mizigo kwa wazazi ambao labda pengine uwezo wao ni mdogo. Badala ya kununua sodo labda watajiwekea hizo fedha na kulipia hao watoto karo za shule. Kwa hivyo, mimi sitazungumza mengi ila nitaunga mkono kwa dhati na pia niwasihii waheshimiwa wenzangu tuunge mkono huu mswada ili kusudi mtoto wa Kilifi aweze kufaidika. Asante sana mheshimiwa Spika.

Hon. Matsaki: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Nimesimama kuunga mkono yale mheshimiwa Koki amezungumza. Kama ulikuwa unamuangalia Koki vile alikuwa anatoa maoni umemuona anazungumza na uchungu. Anazungumza na uchungu kwa sababu ni hali anayoiona kutoka 2013 vile alikuwa anasaidia. Na yeye katika Hoja yake amekuwa anauliza kama itawezekana zile Idara ambazo zinahusika, ya Afya na ya *Gender*, wahakikishe wana mipango mizuri ili watoto wetu waweze kusaidika kiserikali. Kusema kweli, mtu mmoja hawezi kutatua shida zote za Kaunti ya Kilifi. Sio tu kupitisha; tupitische na hata kama itawezekana tujaribu kusukuma ili katika hii *Supplementary Budget* zile Idara mbili waweke pesa ili kwa sasa hawa watoto waweze kusaidika.

Kwa hivyo kama kweli imani zetu ni moja na tunakubaliana mambo haya yawe yatamalizika, basi tuchukue msimamo mmoja na tupitische kama Bunge na huo upande mwengine tuhakikishe wataweka pesa na bajeti ikiletwa hapa wasichana wetu wasaidike. Kusema kweli, wasichana wanaweza kuwa *victims* kwa sababu wengi wametoka katika familia ambazo hazina uwezo; hawawezi kumudu kununua vifaa hivi. Kule tumetoka mama zetu zamani

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

walikuwa wanavaa *mahando* walikuwa wanatumia yale mahando kujisaidia. Si hali nzuri; hii ni karne nyengine kwa hivyo sisi kama ni kubadilisha ni Bunge hili liwe na msimamo mmoja kwamba tunapitisha hii Hoja na baada ya kuipitisha pia tujaribu kadri ya uwezo wetu ili habari ifike kule watuwekee pesa kwa bajeti. *Supplementary* hii ya kwanza ikija iwe na bajeti ya haya mambo ambayo tunazungumzia na ikifikia hapa tupitishie ili mheshimiwa Koki naye roho yake itulie. Asante.

Hon. (Ms.) Messo: Thank you Mr. Speaker, Sir. I stand to support the Motion and congratulate hon. (Ms.) Koki; you are doing a good job. It is so unfortunate that we have a woman representative but she is doing totally nothing. This should be her job. I support hon. Koki and I beg the House to pass the Motion. The only problem with our girls is that some of them are getting pregnant not because of sanitary towels; it is just because they want money. I think we should also have civic education for our girls.

Again, men are also beasts; they are the problem. You know so well that this is a young girl and still going to school yet you seduce her saying she is a 'spring chicken'.

I think we should bring a Bill that any man that will impregnate any school going child should be castrated and that will help us. So hon. Koki, congratulations for the good job; continue doing it and God shall bless you. Thank you.

Hon. (Ms.) Elina: Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono mheshimiwa Koki na ameleta kwa wakati unaofaa kabisa. Wakati huu wa Corona, wengi wa wasichana wetu ni wale wanaopenda kusoma; si kwamba wanakataa kusoma ni matatizo ya kinyumbani tu ndio yanayowarudisha nyuma. Kuna video ya msichana mmoja ambaye alikuwa anazungumzia hisia zake na akasema kwamba angepata yale mahitaji yake hangewacha kusoma lakini shida ni kwamba familia haiwezi kunitengenezea kila ninachokitaka. Wakati huu wa Corona, wasichana wengi wako nyumbani. Kule shuleni walikuwa wakisaidiwa na *well wishers* lakini saa hii wale *well wishers* hawaendi tena kule shuleni maana zimefungwa. Wale wasichana wanasumbuliwa; wengine hata wanasumbuliwa na baadhi ya waheshimwa. Baadhi wako hapa ndani lakini hili jambo tumeliweka kwamba ni bodaboda. Ile video inaonyesha ni ya bodaboda. Msichana alikuwa anapeana kisa chake ya kwamba anawaambia wenzake tusitegemee hawa wavulana wa bodaboda maana hawatusaidii *income* ...

(Hon. Ndago stood on a Point of Order)

Hon. Ndago: Thank you Mr. Speaker. You know that nowadays this honourable House goes live on facebook. It is so unfortunate if our hon. Member who I respect so much because she is a senior Member and also the Chairperson of Gender Committee but if she cannot substantiate...it is a very serious allegation that even some of the hon. Members are dealing with young girls. Maybe she can substantiate or else she withdraws that Statement.

Hon. (Ms.) Elina: Asante mheshimiwa Spika kwa maneno ya mheshimiwa Ndago kama alivyosema yeye pia ni kati ya wale waheshimiwa wadogo. Wakati mwengine yeye mwenyewe huandamana na wasichana wadogo ambao wanataka *school fees* akaja nao mpaka hapa. Yeye hajatuambia anawasaidia vipi; wacha zile *school fees*, kule kando. Hakuna mheshimiwa ambaye hajabeba msichana ambaye anataka kusaidiwa na jambo lolote...

(The hon. Speaker spoke off-record)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Asante mheshimiwa Spika kwa kunijua kwamba ni *withdraw* hayo maneno lakini mume ni mume. *Nimewithdraw* mheshimiwa Spika nashukuru. Asante. Nataka nizungumzie hilo kwa sababu linatutia uchungu.

Kipindi cha huko nyumba tukiwa *County Council* ya Malindi kulikuja kesi fulani kwamba kuna msichana *disabled* ambaye kila mtu alikuwa anamsikitikia yule msichana. Alikuwa anafanya kubebwa apelekwe msituni halafu aregeshwe nyumbani na alikuwa habebwi na mwanamke; anabebwa na mwanamme. Wakati huo huyo mtu alikuwa pia ni kiongozi kwa hivyo sisemi hivyo kwa kuwasingizia bali ni jambo ambalo lishawahi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwa sababu hawa wasichana wale ambao hawajakuwa na umri wa kutosha ndio huwa wanadanganyika sana na hizi pesa kidogo za kununulia sodo. Namuunga mkono mheshimiwa Koki kwa sababu amesema hili jambo lisiwe la mtu binafsi kwa sababu yeye amejaribu hata kulipokuwa na mafuriko Garashi alijaribu kubeba mzigo fulani akapelekea wale wasichana kule. Yeye peke yake hawezi kubeba mzigo wa kaunti na katika kaunti yetu tuna kiongozi wa kina mama na juzi nilishuhudia Tana River kiongozi wao wa kina mama akigawanya sodo. Kwa nini kwetu ilikuwa haiwezi kufanyika? Kilifi hatujasikia kwamba kumekuja hizo sodo.

Kwa hivyo, hilo jambo tulitilie mkazo sisi wenyewe kama serikali ya Kaunti. Ikiwezekana hizi Idara mbili zishirikiane tununue hivi vitu tusaidie watoto wetu. Jana tulizungumzia hospitali. Kilifi yetu iko na shida nyingi na hao wasichana si kwamba ni wadogo hawaelewi kitu; wanaelewa lakini ule upungufu umekuwa mwingi sana. Nafikiri juzi mheshimiwa Koki alileta mjadala hapa kwa sisi wajumbe wa kike kwamba kuna mama alikuwa amezaa kutoka Kaloleni ana watoto wengi na anaomba msaada; tulikaa kama *Members* tukajadiliana naye mpaka akafika katika ile familia. Unajua kuna waheshimiwa wengine mioyo yao ni ya huruma. Mheshimiwa Koki anafanya vile sio ati kwamba ana pesa bali ni ile huruma kwa yule msichana. Kama tutakaa kamati zote mbili za *Gender* na Afya iwe sheria kabisa kwamba Kaunti ya Kilifi watoto kwa kila shule wapelekewe hizo sodo kwa sababu watu wetu wana shida. Hizi pesa ni za serikali na kama raisi mwenyewe alitia saina kinachotushinda sisi katika Kaunti ya Kilifi ni kipi?

Juzi tulikaa na Waziri wetu wa *Gender* akasema shida ya serikali za kaunti wakati wa bajeti pesa zinazopunguzwa ni za *Gender*. Akasema hana pesa hata kuweka mikutano ya vijana kuzungumza nao wanaweza kufanya hili ama lile kwa sababu hakuekewa hata shilingi. Hawa vijana wa Kilifi tutawajibu nini baadaye? Ni jambo ambalo linasikitisha. Inafaa tuisitize hizi Idara mbili tuziekee pesa ili yule mwananchi wa kawaida asaidike. Ni jambo la uchungu lakini hatuwezi kumuachia mheshimiwa Koki peke yake; tumuunge mkono.

Shule ziko karibu kufunguliwa pia na utakuwa ni mzigo kwa mwanafunzi aende shule aonekane vibaya. Mtoto akienda shule aonekana vibaya kesho hatakubali kuenda shule. Kwa hivyo, mimi ningeliomba kama inawezekana tusukume serikali yetu inunue hizo sodo. Kama serikali kuu ilitoa na hatujui za upande wetu zilipelekwa wapi wacha tununue sisi kama serikali ya kaunti. Asante mheshimiwa Spika.

Hon. (Ms.) Maneno: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Hoja hii imeletwa kwa wakati ufaao kwa sababu mheshimiwa Koki amefanya utafiti wa kutosha na kama alivyotujua ameweza kuenda katika wadi kadhaa na akasikia kilio cha wale dada zetu wadogo. Hoja hii tuichukulie kwa uzito. Ni kweli mtoto wa kike Kaunti ya Kilifi anapata shida haswa yule anayetoka katika familia ya kimaskini. Utapata hata hizo sodo ambazo zinagawanywa na *woman representative* ni huko mjini tu lakini kule vitongojini wasichana wetu hawazioni.

Kwa hivyo naunga mkono Hoja hii. Kuna *clip* ambayo ilikuwa inaendelea ambapo msichana alijinyonga kwa sababu alipokuwa kwenye hedhi alichafua ile sketi yake na wavulana darasani wakamcheka. Yule msichana pengine alikuwa na udhaifu wa kile kitu ambacho alikuwa ametumia wakati ule. Kwa hivyo, unaona ya kwamba waliweza kupoteza maisha.

Mini kama Mwenyekiti mdogo wa Kamati ya Afya kama mhashimiwa Matsaki alivyosema tukipitisha leo tutahakikisha Idara ya Afya tutasukuma ili tupate angalau fedha kidogo na mhashimiwa Koki mwenyewe ni mwanakamati; tutaungana pamoja tupate hizo pesa ili tusaidie wale watoto. Asante Bw. Spika.

Hon. Mwarandu: Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity. I rise to make my remarks but before that Mr. Speaker, we are in the midst of COVID-19 pandemic and it has affected many recreational activities. You will realize that in March this year we were supposed to attend the Devolution Conference and it was cancelled due to the pandemic and you understand that the conference also comes with other recreational activities.

Again in August we were supposed to attend the CASA (County Assemblies Sports Association) games and it was also cancelled due to the pandemic. Therefore, I want to bring to the attention of the Members that with the permission from your Office, Mr. Speaker, we have organised recreational activities that it has been and practiced world-over and this is the “Jerusalema Dance Challenge”.

Mr. Speaker, I urge hon. Members to register for those who are interested and the Speaker is willing to assist us and he is also a very good dancer and he is willing to participate. Hon. Members, kindly register...

(Loud consultations)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Member, you should have taken that to a *Kamkunji* (informal meeting)...

Hon. Mwarandu: To register, consult Officer Mr. Omar Chuphi. Now back to the Motion; a line has been drawn between the girl child and the boy child. I have heard one hon. Member saying that men should be castrated. It is very painful; however I support the Motion because the girl child of this county is also very important. We should support them in this very noble exercise and it is not only us as in Kilifi County, the Government has initiated and we also have the Menstruation Health Management Policy 2019-2030 that stipulates that the girl child be given sanitary towels. So I think it is a noble exercise and it is overdue. I support you my sister. Thank you.

Hon. (Ms.) Scholastica: Thank you Mr. Speaker. First, I would like to thank hon. (Ms.) Koki for this Motion. When she was submitting, I could really feel it; it was coming from deep in her heart. Hon. (Ms.) Koki you have a special gift; not all of us can do what you do. I want to support this Motion by saying we really need to educate our girls. We should try and see how we can put a kitty in order for us to go and educate the girls. We should also educate them on adolescent matters. Some of them even fear to speak up when they get their menses especially if it is the first time. Somebody might tell you “*umechafua nguo*” which is quite embarrassing because they do not even know it has started.

So, it is good for us to take some time and educate the girls so that by the time they experience that, they are aware and they know the pros and cons of the same. After that, whenever we are giving them pads they will know exactly what to do as well as take care of themselves.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

You will also find that most of these pads are given to girls in urban areas; the rural area girl is always left out. It is good for us to pass this Motion and to have a sit down with the Committees especially of Gender and Health. Members who are in the Committees both men and women let us embrace this and push for it so that we can get these pads and assist our girls.

It was said that sometimes men provoke the girls; I want to say that we know men are always weak but we should not take it as an excuse. So it is for us ladies to educate our girls so that they can be strong. For a home to stand firm, there always should be a woman. Let us make our girls strong. It is us women that are going to educate these girls and make them know that men are dangerous and they have a weaker part in their life. This will help reduce unplanned pregnancies.

Let us have our own programme and help our children especially in the rural areas. Thank you. I stand to support this Motion.

(Question put and agreed to)

PROCEDURAL MOTION

REDUCTION OF PUBLICATION PERIOD OF THE KILIFI COUNTY FINANCE BILL, 2020

The Leader of Majority (Hon. Mwathethe): Thank you Mr. Speaker. I would wish to move a Procedural Motion:-

THAT, notwithstanding the provisions of Standing Order No. 161 of the Kilifi County Assembly Standing Orders, I move that this House reduces the publication period of the Kilifi County Finance Bill 2020, from seven days to one day.

Mr. Speaker, just briefly, we know that our counties have been straining without money from the National Government and with the county allocations having been signed by the President, we need to start the county financial activities. Waiting for seven good days will be too long for us because we have been waiting for the last three months.

Therefore, I beg that this House reduces the publication period from the seven days to just one day so that things can start rolling. I ask the Chief Whip to second.

(Hon. Mwayaa seconded)

(Question proposed)

(Question put and agreed to)

BILL

First Reading

THE KILIFI COUNTY FINANCE BILL 2020

(Order for the First Reading read- Read the First time and ordered to be referred to the relevant Departmental Committee)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

CONSTITUTION OF AN ADHOC COMMITTEE TO SCRUTINIZE UTILIZATION OF COVID-19 FUNDS IN KILIFI COUNTY

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, before we adjourn I would like to inform you that the Committee on General Oversight is seeking implementation in regards to how the COVID-19 money was spent. These documents shall be made available to the Members. However, as the Chairperson, I wish to direct that there is need to form an ADHOC Committee that will have a session to look into the details together with the experts, then that ADHOC Committee will further report to the General Oversight Committee and then the Committee will consider the report from the ADHOC committee.

The constitution of the Committee will be done through consultations by the Leader of Majority and the Leader of Minority. We shall be an 11 Member Committee. So, hon. Members you have seven days through which you will present the names and then the names will be adopted by the Committee in the next session. The terms of reference will be given to the Committee by the Whole House Committee then they will proceed to ...

(The Speaker spoke off record)

The reason why I opted to do that is we are 54 Members in one Committee; it might not be possible for us to gather facts and thoroughly examine the Executive. It is my hope that the Members who will be in the Committee will do honour and justice to the people of Kilifi and then return to us with a Report that shall be re-considered by the Whole House and then a verdict shall be made.

ADJOURNMENT

Hon. Members, in the absence of any other business on the Order Paper, I move to adjourn this House. Thank you for your patience.

The House rose at 4:30 p.m.